JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI

*(Jeshi la Magereza)*

Anwani ya Simu :" MAGEREZA"
Simu namba: (+255) - 026: 2323300
Fax: (+255)-026: 2323260
Barua pepe: cgp@prisons.go.tz.

OFISI YA KAMISHNA JENERALI WA MAGEREZA
MAKAO MAKUU YA MAGEREZA,
BARABARA YA ARUSHA,
ENEO LA MSALATO,
S.L.P. 1176,
DODOMA.

# TAARIFA KWA UMMA KUHUSU NAFASI ZA AJIRA 700 ZA KUJIUNGA NA JESHI LA MAGEREZA KWA MWAKA 2021

**Septemba 27, 2021 - DODOMA**

Kufuatia mkakati wa Serikali wa kuimarisha utendaji wake, imetoa fursa ya ajira kwa Wizara na taasisi mbalimbali za Serikali katika nafasi mbalimbali kwa kadri ya mahitaji yake. Kwa muktadha huo, Kamishna Jenerali wa Jeshi la Magereza, Meja Jenerali Suleiman Mungiya Mzee anatangaza nafasi za ajira 700 za kujiunga na Jeshi la Magereza kwa mwaka 2021 kwa wale wenye elimu ya kidato cha nne na wale wenye taaluma/ujuzi mbalimbali kama zilivyoainishwa katika tangazo hili.

**(a) Sifa za muombaji wa elimu ya kidato cha nne ;**

- Awe ni raia wa Tanzania
- Awe amemaliza kidato cha nne na kupata ufaulu wa daraja la IV (points 28-32)
- Awe na umri kati ya miaka 18 – 25
- Awe na siha njema
- Awe kwenye mafunzo au awe amefuzu tayari mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)
- Asiwe amewahi kuajiriwa serikalini
- Asiwe ameoa/ kuolewa



Scanned with CamScanner

- Awe na nidhamu na tabia njema na awe hajawahi kupatikana na hatia mahakamani na hajawahi kufungwa
- Awe na urefu usiopungua futi 5'4 kwa wanawake na futi 5'7 kwa wanaume

(b) Sifa za muombaji kwa wale wenye taaluma/ujuzi;

- Awe ni raia wa Tanzania
- Awe na umri kati ya miaka 18 -33
- Awe na siha njema
- Awe kwenye mafunzo au amefuzu tayari mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)
- Asiwe amewahi kuajiriwa serikalini
- Asiwe ameoa/Kuolewa
- Awe na nidhamu na tabia njema na awe hajawahi kupatikana na hatia mahakamani na hajawahi kufungwa
- Awe na urefu usiopungua futi 5'4 kwa wanawake na futi 5'7 kwa wanaume

Kwa wale wenye taaluma/ujuzi, wawe na taaluma katika fani zilizoainishwa katika kiambatanisho namba 1 kilichoambatanishwa katika tangazo hili.

Aidha, barua za maombi ni lazima ziambatanishwe na nakala zifuatazo;

- Nakala ya cheti cha kuzaliwa (Birth Certificate)
- Nakala ya cheti cha kuhitimu elimu ya kidato cha nne au cha sita
- Nakala ya cheti cha kumaliza shule (Leaving Certificate)
- Cheti cha uthibitisho wa siha njema kutoka kwa mganga wa serikali
- Nakala ya kitambulisho au namba ya utaifa (NIDA)
- Nakala ya cheti cha kufuzu mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa (JKT)
- Picha nne (4) za passport size
- Nakala za cheti cha taaluma/ ujuzi husika kinachotambulika na mamlaka za elimu nchini (kwa wale wenye taaluma/ ujuzi)
- Barua ya utambulisho kutoka kwa Afisa Mtendaji wa Kijiji/Mtaa
- Wasifu (Curriculum Vitae – CV) – (Kwa wale wenye Taaluma/ujuzi tu)



Scanned with CamScanner

Utaratibu wa kutuma maombi ni kama ifuatavyo;

- Kwa wale wote waombaji wa elimu ya kidato cha nne, maombi yao yatumwe kwa Mkuu wa Gereza la Wilaya husika, aidha, kwa wilaya zote ambazo hazina Gereza maombi yao yatumwe kwa Mkuu wa Gereza lililo jirani kwaajili ya kujadiliwa katika Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya na baadae mkoani. Barua zote za maombi zitumwe kwa njia ya posta au barua pepe, hakuna barua itakayopokelewa kwa njia ya mkono.
- Kwa wale wote wenye taaluma/ujuzi maombi yao yatumwe kwa Kamishna Jenerali wa Magereza, Barabara ya Arusha, Eneo la Msalato, P.O.Box 1176, Dodoma au kwa kutumia barua pepe training@prisons.go.tz au kwa njia ya EMS.
- Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 10. 10. 2021

Inakumbushwa kuwa ni kosa la jinai kuwasilisha nyaraka za uongo (Forged documents), hivyo,hatua kali za kisheria zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani kwa wale wote watakaobainika kufanya hivyo, aidha, inakumbushwa pia kwa yoyote yule atakayefanya mchakato huo kinyume cha utaratibu, ama kwa kutaka kusaidiwa na mtumishi wa Jeshi la Magereza au mtu mwingine yoyote na kutapeliwa fedha zake au utapeli mwingine unaofanana na huo, itahesabika wote wawili ni wakosefu kwa mujibu wa sheria. Asanteni.

SACP – JUSTINE M KAZIULAYA

(MSEMAJI WA JESHI LA MAGEREZA)



Scanned with CamScanner

## ORODHA YA TAALUMA/UJUZI UNAOHITAJIKA ( UK.4-6 )

Software engineering – (Degree)

Data base developers or data base programmer – (Degree)

Website design and web developers – (Degree)

Cyber security engineering or network administration and security – (Degree)

Office machine mechanical (level III, II)

Ualimu wa Hesabu – (Degree/ Diploma)

Ualimu wa Fizikia – (Degree /Diploma)

Ualimu wa Kifaransa – (Degree/Diploma)

BSC. Agriculture general

BSC. Crop science and production

BSC. Agronomy

BSC. Horticulture

Diploma in crop production

Diploma in animal health production/Diploma in animal production

Diploma in agro mechanization

Tractor driving- (Licence class G)

Diploma in soil and irrigation engineering

Diploma in forest conservation /management

Diploma of beekeeping

BSC. Agricultural economics and agribusiness



Scanned with CamScanner

Diploma in fisheries management

Utengenezaji samani (cabinet making) – (level III, II)

Ubunifu na ushonaji (Design sewing and cloth technology) - (level III, II)

Utengenezaji sabuni (soap making) - (level III, II)

Bidhaa za ngozi (leather production technology) – (level III, II)

Ufumaji vikoi (hand loom weaving) - (level III, II)

Mitambo (mechanical technician) - (Diploma)

Umeme wa viwandani (Industrial electrical installation) – (Diploma)

Kemikali (chemical and processing engineering) - (Degree)

Uhandisi madini (mining engineering) - (Degree)

Highway engineering- (Degree)

Structural engineering- (Degree)

Architects- (Degree/Diploma)

Quantity survey- (Degree)

Land surveyors-geomatics- (Degree/Diploma)

Land surveyors-geoinformatics- (Degree)

Land valuer and estate manager-(Degree)

Construction management- (Degree)

Land scape architect- (Degree)

Civil works- (level III, II)

Welding –(level – III, II)

Aluminium works – (level III, II)



Scanned with CamScanner

Steel fixers- (level III, II)

Uganga- (Diploma)

Famasia-(Diploma)

Maabara- (Diploma)

Uuguzi – (Diploma)

Wataalamu katika miradi- (Degree)

Wataalamu katika sera-(Degree)



Scanned with CamScanner